*Ukweli Hauna Kutu*

# Pambazuko

Toleo Namba 024 Jumatatu Desemba 26-Januari 1,2023

# Siku aliyozaliwa Yesu bado Kitendawili

- *Ni Desemba 25, Januari 6 au 7?*



## Taharuki kusudio la Papa kujiuzulu

Uk. 5

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Heri ya mwaka mpya






## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.
- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## *NUKUU*



***KUNA njia moja tu ya kuepuka kukosolewa, ukiona usiseme kitu, ukisema usiandike kitu, usifanye kitu na wala usiwe chochote. Hapo utaweza kuepuka lawama pia na kutokwaza wengine – Aristotle, Mwanafalsafa wa Ugiriki***

# Kuwa tayari huondoa hofu kuu

**Na Plato Hekimachius**

KUNA mambo yanatokea mara kwa mara na kujijengea kanuni kuwa ni ya kawaida na yataendelea kutokea.

Yamekuwapo katika harakati za kupigania uhuru, yakaendelea baada ya uhuru na yanaendelea hata sasa, zaidi ya nusu karne tangu Tanzania ipate uhuru. Haya mambo yanahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu na yakubaliwe kuwa ni sehemu muhimu ya historia ya ukombozi. Nitajadili matatu kwa ufupi.

Kwanza, ukipenda madaraka, usiogope kifungo.

Ukiwa nje ya mfumo na unapigania ili uingie madarakani, ni bora kujiandaa kisaikolojia kuwa kifungoni. Aidha, ukiwa madarakani na unapenda hayo madaraka, ujiandae kisaikolojia kuwa ipo siku utajikuta kifungoni ukiwa madarakani au hata baada ya kutoka madarakani.

Uwepo wa kinga za kisheria ndani ya katiba za nchi, hauzuii mtu kuwekwa kifungoni. Hii ni kwa sababu hata wale wasiokuwa madarakani, wana kinga isiyoandikwa kwenye katiba, lakini walio madarakani huzipuuza na kuwaweka kifungoni.

Mnyumbuliko huu ndio hujenga mazoea ya unasaba kati ya kifungo na madaraka. Viongozi wa kisiasa waliofanikiwa katika maisha ya kisiasa ni wale waliokubali kuwa kifungo na madaraka ni ndugu wa damu.

Pili, ukipenda kutetea haki, kubali kudhalilishwa.

Haki ni kinyume cha dhuluma. Kwa hiyo ukitetea haki unaingia katika vita na dhuluma. Mfumo wa dhuluma una watetezi wake pia na wako katika tasnia zote. Kwa hiyo ukiigusa dhuluma, watetezi wake huinuka na kupambana na watetezi wa haki.

Njia maarufu ya kukabiliana na watetezi wa haki ni kuwadhalilisha kwa uwongo, kuwaita majina mabaya, na hata kuwatishia kifo.

Hali hii huwaweka watetezi wa haki wote kuwa tayari kutukanwa na kudhalilishwa wakati wowote. Udhalilishaji wa watetezi unahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu kwa sababu ni sehemu muhimu isiyobadilika.




*Pingu*

Watetezi wa haki duniani kote yawapasa kujiandaa kisaikolojia kukabiliana na kuizoea hali hii.

Tatu, ukipenda habari za uchunguzi, uwe tayari kufungiwa.

Habari za uchunguzi katika tasnia ya habari ni kiungo muhimu kinachoongeza heshima ya tasnia hiyo. Lakini, heshima hiyo ina gharama kubwa kwa waandishi.

Serikali nyingi pamoja na kujinadi kuwa za kidemokrasia, lakini linapofika suala la habari za uchunguzi, serikali hizo hutumia sheria kandamizi kuzuia habari hizo.

Mbinu zinazotumiwa na serikali hizo ni pamoja na utaratibu wa 'kulesenisha' habari, kufanya usanii wa kukiri uwepo wa sheria kandamizi, lakini bila kuchukua hatua ya kuzifuta, na kutumia wana habari wenyewe kuwa wasimamizi wa mifumo kandamizi ya habari za uchunguzi. Kilele cha dhuluma dhidi ya habari za uchunguzi ni uwepo wa kisingizio cha uchochezi na kuhatarisha usalama wa nchi.

Kwa hiyo, ukiwa mwandishi wa habari za uchunguzi ni vyema kuwa tayari kufungiwa, kufungwa, kufilisiwa na kuvurugwa kimapato.

# Taharuki kusudio la Papa kujiuzulu

WIKI iliyopita taharuki ilisambaa duniani kutokana na taarifa kwamba, tayari Papa Francis alikuwa ameandika barua ya kusudio la kujiuzulu kwa sababu za kiafya au matatizo mengine.

Taarifa hizo zilionyesha kwamba, Papa aliandika barua hiyo miaka tisa iliyopita, yaani mwaka 2013, mara tu baada ya kuchaguliwa kuwa kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki duniani.

Papa Francis alifichua taarifa hizi wakati akihojiwa na waandishi Julian Quiros na Javier Martínez-Brocal, wa gazeti la ABC la huko Hispania na hakueleza sababu za kufanya hivyo.

Baadaye, taarifa hizo zilithibitishwa na chapisho kwenye tovuti ya Vatican, likiwa na kichwa cha maneno; "Nimekwishaandika barua ya kusudio la kujiuzulu kwa sababu za kiafya."

Papa ni Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Kanisa lenye kuongozwa na kisheria na kikatiba.

Kwa mujibu wa Sheria za Kanisa Katoliki (1983) ibara ya 335, kiti cha Papa kinapokuwa wazi "hakuna mabadiliko yoyote yanayopaswa kufanywa katika mfumo wa uendeshaji wa Kanisa; badala yake, katiba maalum inayosimamia kipindi cha mpito inapaswa kufuatwa." Katiba hiyo ilitungwa mwaka 1996 na Papa Yohanne Paul II.

Swali linaloulizwa na wadadisi wa masuala ya uendeshaji wa Kanisa Katoliki ni hili: "Kwa nini Papa Francis alilazimika kuandika barua ya mwongozo wa ziada kuhusu kipindi cha mpito, wakati tayari Kanisa linayo Katiba mahsusi?"

Mtaalam wa masuala ya uongozi wa Kanisa Katoliki, Brian Dive, wa Uingereza, amejaribu kujibu swali hili kupitia kitabu chake, "Accountability and Leadership in the Catholic Church: What Needs to Be Improved (2020)." Dive anasema yafuatayo:

Kwamba, muundo wa uongozi wa Kanisa Katoliki haujasanifiwa vizuri; Papa ndiye mtu pekee mwenye mamlaka rasmi juu ya maaskofu; Kuna maaskofu wengi, wapatao 5,300; Papa hawezi kuwasimamia wote, moja kwa moja na kwa ufanisi.


*Papa Francis*

Kwamba, kuna viongozi wengine 700 wanaoripoti kwa Papa moja kwa moja; Hawa ni wakuu wa mashirika ya kidini, na wakuu wa idara mbalimbali za Kuria ya Roma (hili ni sawa na Baraza la Mawaziri la Papa); Kwa hiyo, papa anapaswa kusimamia, kuelekeza na kusikiliza watu 6,000 kwa mpigo.

Kwamba, Papa hawezi kufanya kazi hii kwa kasi na ufanisi; Kuna ombwe la uongozi; Kuria ya Roma, yenye mamlaka ya kumshauri Papa, imejitwalia madaraka, pasipo uhalali, ya kuwasimamia maaskofu; hivyo, kuna kuna ngazi ya uongozi, yenye mamlaka kamili ya kuwasimamia maaskofu na kuripoti kwa Papa inakosekana.

Historia inaonyesha kuwa Papa Paul VI aliwahi kuandika barua ya kujiuzulu na "kuificha" kwa muda mrefu zaidi na inaelezwa ilipatikana baada ya kifo chake Agosti 6, 1978. Alichaguliwa kuwa Papa Juni 21, 1963.

# Hewa ya ukaa yawapa Sh bilioni 10 Katavi

**Na Deusdedith KAHANGWA**

BIASHARA ya hewa ya ukaa imewanufaisha wananchi wa vijiji vinane wilayani Tanganyika, mkoani Katavi – kwa kupata shilingi bilioni 10.

Walionufaika na biashara hiyo ni wananchi kutoka vijiji vya Bujombe, Kagunga, Kapanga, Katuma, Lugonesi, Lwega, Mpembe, na Mwese. Hadi mwaka 2022, inakadiriwa kuwa vijiji hivi vinao wakazi 34,000.

Taarifa iliyopatikana kwa Pambazuko lililotembelea vijiji hivyo inaeleza kuwa katika mwaka wa 2022 vijiji hivyo vimevuna shilingi 10,3000,000,000. Huu ni wastani wa shilingi 3,029,412 za Tanzania kwa kila mwanakijiji.

Mradi unatekelezwa na kampuni ya Carbon Tanzania kwa kushirikiana na wananchi kutoka vijiji hivyo.

Mradi huu wa kufyonza hewa ya ukaa kwa kutumia misitu iliyo kwenye Milima ya Ntakata, ni mradi wa kutunza msitu asilia wenye eneo la hekta za mraba 216,994. Mkataba kati ya Carbon Tanzania Ltd na wanavijiji ulisainiwa Oktoba 3, 2018.

"Mkataba huu unasema kuwa wananchi na Kampuni ya Carbon Tanzania watakuwa wanagawana mapata kwa kuzingatia kanuni ya nusu kwa nusu," anaeleza David Berrof, meneja shughuli wa mradi.

"Mwezi Julai mwaka huu, vijiji vilikabidhiwa hundi ya shilingi 2,300,000,000 za Tanzania. Na Desemba mwaka huu, vijiji vimekabidhiwa hundi ya shilingi 8,000,000,000 za Tanzania," anaeleza Jo Anderson, Mkurugenzi wa Fedha wa Mradi.

Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu pato la mwaka kwa kila mkoa katika mwaka 2020 zinaonyesha kuwa, Mkoa wa Katavi una pato la shilingi 1,997,154,000,000 za Tanzania kwa mwaka. Hii ni sawa na asilimia 1.3 ya pato la Taifa, sawa na wastani wa shilingi 2,478,206 za Tanzania kwa kila mtu kwa mwaka.



*Frank Kweka*

Hivyo, kipato cha wananchi walio kwenye mradi kinazidi kipato cha wananchi walio nje ya mradi kwa wastani wa shilingi 551,206 za Tanzania.

Mkataba wa mradi kati ya Carbon Tanzania Ltd na wanavijiji, unasema kuwa malengo ya mradi ni pamoja na: kuviwezesha vijiji kupata kipato kutokana na mauzo ya "hewa ya ukaa" kwa kupuguza uzalishwaji wa hewa ya ukaa.

Meneja wa mradi huo Frank Kweka anasema mkataba huo unasema kwamba, majukumu muhimu ya Carbon Tanzania ni kuendesha mradi; kutafuta wanunuzi sahihi wa "hewa ya ukaa"; na kulipa asilimia 50 ya mapato kwa vijiji, vitakavyoamua jinsi ya kuzitumia katika miradi ya maendelao.

Aidha, mkataba unawataka wanavijiji kuhakikisha matumizi bora ya ardhi; na kuzuia ukatwaji wa miti. Na majukumu ya pamoja ni pamoja na kuheshimu sheria za misitu.

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Salehe Mhando, pamoja na Afisa Sheria wa Wilaya ya Tanganyika, Mboki John, waliushuhudia mkataba husika kwa kuusaini. Tangazo la serikali Namba 636/2022 limetaja kanuni za kusimamia biashara hii.

# Eacop: Tunajali zaidi haki



*Moja ya nyumba wanazojengewa watu waliopoteza nyumba zao kwenye mradi huo.*

**Na Mwandishi Wetu, Manyara**

MRADI mkubwa wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi wa Afrika Mashariki (Eacop) unatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia haki za binadamu kwa watu wote wanaoguswa na mchakato wa kukamilisha mradi huo.

Pamoja na kuzingatia haki za binadamu, Eacop inajali haki na maisha ya jamii za pembezoni ambazo zinatajwa kuwa na mahitaji maalum.

Meneja Mkuu wa Eacop kwa upande wa Tanzania, Wendy Brown, hivi karibuni akiwa Kitongoji cha Napilikunya, Manyara alisema kampuni hiyo ya bomba la mafuta inafuata taratibu zote kuhakikisha kwamba watu wanaoguswa na mradi huo, hawapotezi hadhi ya maisha yao wakati wa kutekelezwa kwa shughuli za kutandaza bomba hilo la mafuta unaohusisha nchi mbili za Afrika Mashariki; Tanzania na Uganda.

Wendy alisema kampuni yake imejizatiti kufuata sheria zote za Serikali ya Tanzania na taratibu za kimataifa, hasa Benki ya Dunia katika kutekeleza shughuli zake bila kuathiri maisha ya watu wanaoguswa na mradi huo mkubwa na wa kimkakati.

Eacop imekuwa katika mazungumzo ya muda mrefu na jamii ya watu wa kabila la Akie wanaoguswa na mradi huo wa bomba ili kupata muafaka wa namna ya kuzingatia maisha, mila na desturi zao kabla ya kuanza utekelezaji.

Wiki iliyopita, Eacop na uongozi wa serikali na jamii ya Akie waliingia mkataba wa mpango kazi na makubaliano ya ridhaa huru ambapo jamii hiyo itapata fursa zinazotokana na kuguswa na mchakato wa kutandaza bomba hilo linalopita kwenye baadhi ya maeneo yao.

Mshauri wa Eacop kuhusu jamii za pembezoni, Dkt. Elifuraha Laltaika alisema kwa furaha, “Ninajivunia ukweli kwamba Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi chache katika ukanda wa Afrika kutekeleza ridhaa huru ya mpango mpya na kabambe wa sheria za kimataifa unaohitaji ushirikishwaji wenye tija kwa jamii za pembezoni kabla ya kutekeleza mradi katika ardhi ya Akie.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kiteto, aliipongeza Eacop kwa ushirikishwaji wenye tija ambao umefanya shughuli za mradi wa bomba kufanyika bila kizuizi katika wilaya hiyo kwa kuwa imefuata vigezo vya kimataifa.

Ridhaa Huru ya Uelewa Kabla ya Utekelezaji wa Mradi (FPIC) ni kigezo muhimu kilichowekwa na mashirika ya fedha ya kimataifa na sheria za haki za binadamu ili kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ili kulinda ardhi na urithi wa asili wa jamii za pembezoni.

# Haki: Chemchem ya baraka

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

JE, safari ya kusimamia na kutenda haki ilikuwaje ndani ya jamii yetu katika mwaka 2022?

Hakuna jambo la hatari na ambalo hunyang'anya amani na furaha ya kila raia katika taifa kama kuvurugika kwa mfumo wa utoaji haki.

Hali ya jinsi hiyo inapokuwepo katika jamii husababisha maumivu na machungu mengi yanayobeba machozi na hata kumwagika damu za watu wasiokuwa na hatia.

Kuvurugika kwa mifumo ya utoaji haki kunatokana na nguvu ya uovu, hujeruhi vibaya utu wetu wa asili. Biblia inatuambia kuwa tayari utu ule wa asili ulikwisha vurugwa na ibilisi kupitia kwa njia ya Adamu na Hawa.

Kwa imani ya kikristo, ukombozi katika Kristo ulililiponya jeraha alilotutia shetani, lakini kovu lingalipo (fundisho la Baba wa Kanisa Askofu Augustino wa Hippo). Kwa kifupi tumepewa nguvu za kushinda uovu kwa nguvu ya ukombozi wa nafsini alionifanyia Kristo.

Pale ambapo neema haitupi ushindi dhidi ya uovu, basi ni muhimu iwepo sheria ya kuwadhibiti waovu. Kwa hiyo, mfumo wa sheria ndio mfumo wa wazi na mpana wa utoaji haki na ambao umebaki kuwa tumaini katika mataifa.

Watawala wanaosimamia mfumo wa sheria wasipokuwa watu wa haki, hutumbukiza taifa zima katika mfumo wa uovu.

Kwa upande mmoja, ni muhimu kukumbusha mihimili kama Bunge juu ya ulazima wa kujenga dhamira safi katika kutunga sheria. Sheria za haki hutungwa ili kulinda mambo yaongezayo amani na furaha ya taifa na kuzuia mambo yaondoayo amani na furaha yao.

Bado hatujasahau mchakato wa kupata katiba mpya Tanzania ulivyokwenda wakati ule na jinsi tunavyoendelea kupigana mateke juu ya jambo hilo.

Tunaliombea Bunge kwa sababu ndipo



*Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma*

inapotakiwa kukaa hekima ya kuona na kutunga sheria zinazoletea baraka taifa.

Yawezekana zikawepo sheria nzuri, lakini vyombo vinavyosimamia ufafanuzi na utekelezwaji wake vikawa vimegubikwa na uovu.

Kwa sababu hiyo, haki haitolewi ipasavyo na inapotolewa hutolewa kwa kupindisha sheria na hukumu. Dhamira safi katika kutawala na kusimamia utoaji haki ni chimbuko la baraka na fahari ya taifa.

Sheria nzuri katika taifa ni msingi wa baraka. Usimamiaji wake ukiwa mzuri ni baraka juu ya baraka na pia ni fahari kwa taifa. Usimamiaji mbaya hupeperusha bendera ya uovu na hivyo kuliletea taifa laana na aibu.

Haki ni chimbuko la amani na furaha ya kila mtu. Haki ni nguzo ya kati inayoshikilia baraka na fahari ya taifa.

Pasipo Haki hakuna maendeleo ya kweli! Bunge, na watawala, na mahakama kwa dhati wakijifunga mshipi wa Haki ndipo baraka itakuja juu ya taifa letu mpaka tushangae.

Nawatakia Noeli ya furaha na mwaka mpya 2023 wenye baraka.

Mezani kwa Chahali



**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Kero umeme na vinasaba CCM

MAKALA haya ni ya mwisho kwa mwaka huu 2022, ambapo makala ijayo itakuwa ya kwanza kwa mwaka 2023.

Mwaka huu unamalizika huku kukiwa na vilio kutoka kona mbalimbali za Tanzania kuhusu mgao wa umeme.

Hata hivyo ni vigumu kuhitimisha kuwa mgao huo wa mwaka huu ni "mkali zaidi" kulinganisha na miaka mingine. Ugumu huo unatokana na sababu kadhaa, lakini kubwa ya msingi ni ukweli kwamba tatizo la kukatika umeme mara kwa mara, na mgao wa umeme kwa ujumla, ni kitu kilichozoeleka miongoni mwa Watanzania.

Na kuzoeleka huko kunasababisha kutokuwa na umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi za - kwa mfano, jiji la Dar lilikumbwa na mgao wa umeme mara ngapi katika mwezi huu wa Desemba, achilia mbali mwaka mzima wa 2022..

Lakini hata kama takwimu zingekuwepo, zingesaidia nini kama hakuna jitihada za makusudi za kulifanya tatizo la mgao wa umeme kuwa historia.

Majuzi, baada ya shughuli ya kuruhusu maji kuingia kwenye Bwawa la Nyerere, gazeti moja la kila siku lilieleza kwamba tatizo la mgao wa umeme litakuwa historia pindi mradi huo ukikamilika.

Hata hivyo, kauli hiyo imekuwa ikijirudia miaka nenda miaka rudi. Miaka michache iliyopita, Watanzania waliambiwa kuwa pindi mradi wa gesi ya Mtwara ukikamilika, mgao wa umeme utakuwa historia. Cha kushangaza, sasa hata hawaongelei tena mradi huo, wamehamia kwenye Bwawa la Nyerere.

Tatizo la umeme lina asili ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kwa upande mmoja awamu mbalimbali za utawala wa chama hicho zimeshindwa kupambana na rushwa na ufisadi ambao



*Waziri wa Nishati, January Makamba*

hasa ndio unaosababisha sintofahamu kwenye sekta ya umeme.

Siyo siri kwamba uwepo wa mgao wa umeme unawatajirisha watu wanaouza jenereta. Na yayumkinika kuamini kuwa "matajiri wa mgao wa umeme" wataendelea kupambana kuhakikisha kuwa tatizo la mgao wa umeme linakuwa endelevu ili wao wazidi kuneemeka.

CCM pia inabeba lawama kwa sababu imewekeza nguvu nyingi katika kuwaaminisha Watanzania kuwa "tupo vizuri" ilhali Watanzania hao wana akili timamu za kubaini kuwa "kuna walakini" (kwa mfano kwenye hili janga la mgao wa umeme).

Nihitimishe kwa kuwatakia Watanzania wenzangu heri ya mwaka mpya 2023, nikitarajia kuwa mwaka huo utakuwa na heri na fanaka kwenu na kwa Tanzania yetu.

# Siku aliyozaliwa Yesu bado Kitendawili

**Na Mwandishi WETU**

WANAZUONI wengi duniani, bado wanaumiza vichwa kuhusu tarehe sahihi aliyozaliwa Yesu Kristo, ambaye ni Nabii wa Wakristo.

Miaka nenda rudi, vitabu vingi vimeandikwa na makundi ya wanazuoni wa dini na historia kuanzia Mashariki ya Kati, Amerika, Ulaya, Afrika na bado hadi leo, maandishi mapya yanaendelea kuchapishwa juu ya kuzaliwa kwa Yetu Mnazareti.

Mjadala huo upo na hakika hautakoma kwani wanaoandika wanapingana kwa hesabu na historia. Wameshindwa kupata tarehe hasa aliyozaliwa Yesu ambaye pia huitwa Masihi.

Miaka 2000 iliyopita, mtawala wa tano wa Wayahudi, Pontio Pilato alimuuliza Yesu wa Nazareti swali lifuatalo: "Ukweli ni kitu gani?" Aliuizwa swali hili wakati anakaribia kupewa hukumu ya kuwambwa msalabani baada ya kukamatwa akituhumiwa kujiita "Mfalme wa Wayahudi."

Yesu hakujibu swali hili. Na hadi leo, kambi kadhaa za wanazuoni zinazidi kuvutana kuhusu jawabu sahihi kwa swali hili.

Mfano mzuri wa mvutano huo unajitokeza katika mjadala kuhusu "siku ya kuzaliwa kwa Yesu wa Nazareti."

Mpaka leo, kuna siku tatu tofauti zinazotajwa kama siku za kuzaliwa kwa Yesu. Kuna Desemba 25, Januari 6 na Januari 7. Ufafanuzi wa utata huu unafuata.

Tuanze na Desemba 25. Haya ni mawazo ya Mtakatifu Hippolytus wa Roma.

Kwa mujibu wa utafiti wa Profesa Andrew McGowan wa Chuo Kiukuu cha Melbourne, mwaka 204BK, Hippolytus aliandika kwamba, "Tarehe ya kuzaliwa Yesu, Bethlehem, ni Desemba 25."

Hippolytus alianzia kwenye tukio la Malaika Gabriel kumtokea Zakaria hekaluni na kumwambia kwamba mkewe Elizabeth angepata mimba na kumzaa Yohane.

Zakaria alikuwa kwenye ibada ya malipizi ya dhambi. Kwa mujibu wa

*Inaendelea Uk. 11*



*Yesu Kristo*

# Siku aliyozaliwa Yesu bado Kitendawili

kalenda ya Kiebrania ibada hiyo ilifanyika tarehe Julai 10 kila mwaka wa Kiyahudi.

Ulinganisho wa kalenda ya kale ya Wayahudi na kalenda ya kisasa unaonyesha kuwa siku hiyo ni sawa na Septemba 24 ya siku hizi. Hii maana yake ni kwamba Elizabeth alianza ujauzito wa Yohane Septemba 24.

Kwa mujibu wa uchambuzi wa Hippolytus, miezi sita baadaye malaika Gabriel alimtokea Bikira Maria na kumwambia atapata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Hivyo, ujauzito wa Yohane ulioanza Septemba 24 uliutangulia ujauzito wa Yesu kwa miezi sita. Hii maana yake ni kwamba, mimba ya Yesu ilianza Machi 25 na akazaliwa miezi tisa baadaye, yaani Desemba 25, anahitimisha Hippolytus.

Lakini, bado wapo Wakristo waliopinga tafsiri ya Hippolytus. Walihoji uhalali wa hesabu zake, wakitaka awaonyeshe hiyo miezi tisa ilikuwa na jumla ya siku ngapi.

Hawa wenye kupinga Krismas ya Desemba 25, huadhimisha Krismas ya Januari 7. Ni wafuasi wa Mfamle Julius Kaizari wa dola ya Kirumi. Sababu za upinzani wao zinafuata.

Katika mwaka 46KK Julius Kaizari aliunda kalenda iliyotokana na imani kwamba mzunguko wa dunia unachukua siku siku 365 tu.

Lakini, baadaye wanasayansi waligundua kuwa mzunguko wa dunia huchukua siku 365 na robo.

Robo nne zinaunda mwaka mmoja. Hii maana yake ni kwamba, kila baada ya miaka mitatu, yaani katika mwaka wa nne, mzunguko wa dunia huchukua siku 366.

Miaka mitatu huitwa miaka mifupi, na mwaka wa nne kuitwa mwaka mrefu. Mwaka mrefu hugawanyika kwa namba "nne."

Kwa mujibu wa "Kalenda ya Julius" mwaka wenye siku 365 una miezi 12;



*Yesu Mnazareti*

ambapo miezi minne ina siku 30, kila mmoja; miezi saba ina siku 31, kila mmoja; na mwezi Februari una siku 28.

Hesabu hizi hazihusishi siku 365 pekee kati ya siku 365 na "robo" za mzunguko wa dunia.

Hivyo, kila baada ya miaka minne, "Kalenda ya Julius" ikawa inapoteza siku moja kamili.

Kwa ajili ya kuondoa dosari hii, katika kila mwaka mrefu, Julius aliamua kuongeza siku moja kwenye mwezi wa Februari, ili uwe na siku 29, na hivyo kukamilisha siku 366 za mwaka mrefu.

Kalenda hii ina miezi minne ya siku 30, miezi saba ya siku 31, mwezi Februari wa siku 28 katika mwaka mfupi, na mwezi Februari wenye siku 29 katika mwaka mrefu. Huitwa "Kalenda ya Julius".

Baadaye wanasayansi waligundua tena kuwa mzunguko wa dunia hauchukui siku "365.25" pekee, bali huchukua siku "365.24218967."

Hapa kuna tofauti ya siku "0.00781033," sawa na dakika "11.2468752." Yaani, kimakosa, "Kalenda ya Julius" ilikuwa imeongeza dakika

*Inaendelea Uk. 12*

# Siku aliyozaliwa Yesu bado Kitendawili

*Inatoka Uk. 11*

"11.2468752" katika mwaka mzima.

Kanisa Katoliki lilianza kutumia kalenda ya Liturijia inayofuata mantiki ya "Kalenda ya Julius" mwaka 325.

Lakini, mwaka 1582 Papa Gregory wa 13 aligundua makosa hayo yaliyo kwenye "Kalenda ya Julius." Hivyo, Papa akakosoa dosari husika kwa kuunda kalenda mpya, ikaitwa "Kalenda ya Gregory".

Baadhi ya Wakristo waliikataa mantiki iliyoongoza utengenezwaji wa "Kalenda ya Gregory" na kuendelea kutumia "Kalenda ya Julius."

Hivyo, tangu mwaka 325 hadi leo imepita miaka 1697. Kwa kuzingatia tofauti ya siku "0.00781033" tulizoona hapo awali, hesabu ya kuzidisha inaonyesha kwamba "Kalenda ya Gregory" inaitangulia "Kalenda ya Julius" kwa siku "13.25413001." Huu ni wastani wa siku 13 na robo.

Hivyo, wakati Wakristo wanaofuata "Kalenda ya Gregory" wanaposherehekea Krismas ya Desemba 25, wale wanaofuata "Kalenda ya Julius" watasubiri hadi Januari 7, yaani siku 13 baadaye.

Lakini pia, kuna Wakristo wanapinga Krismas ya Desemba 25 na kukataa Krismas ya Januari 7, wao wanaadhimisha Krismas ya Januari 6.

Kitabu cha "New Advent Encyclopedia," kinasema hawa wanaoamini Yesu alizaliwa Januari 6 ni wafuasi wa Clement wa Alexandria, nchini Misri.

Clement alionyesha kwenye kitabu chake kiitwacho "Stromata," kwamba Yesu alizaliwa "Januari 6." Baadhi ya Wakristo walikubaliana na Clement hadi leo.

Kutokana na mkanganyiko huo wa siku aliyozaliwa Yesu Mnazareti, ndiyo maana yapo maeneo duniani yanaadhimisha kuzaliwa kwake Desemba 25, wengine Januari 6 na wapo wanaofanya kumbukizi Januari 7.



*Nabii Yesu*

Mchungaji wa Kanisa la Mfalme Yesu lililoko Mwanjelwa, Mbeya, Ibarhim Kalembo akizungumza na Pambazuko kuhusu tarehe hasa ya kuzaliwa Yesu Kristo, alisema ni kweli kuna tofauti kulingana na maeneo husika, lakini uhakika kabisa haueleztwi kinagaubaga na Biblia yenyewe.

Amesema katika vitabu vingi vya vya Injili, ambavyo vikisomwa kwa pamoja, kuna utata wa siku ya kuzaliwa Yesu Kristo, kwani haitamkwi wala kuelezwa kwa uwazi.

"Hata wewe ni Mkristo, umewahi kusoma ama kuelezwa mahali kwamba Desemba 25 ndiyo hasa alizaliwa Mwana wa Mungu (Yesu), hakuna, lakini watu waliamua iwe hiyo Desemba 25 kwa wengi, pamoja na kwamba wapo wanaopinga tarehe hiyo," ameongeza mchungaji huyo ambaye amesema ana shahada ya uzamili katika teolojia.

Anaeleza kuwa mvutano wa siku ya kuzaliwa Yesu huenda usifike mwisho na labda unaweza kutatuliwa na Yeye mwenyewe siku atakaporejea na endapo atatoa nafasi ya kuulizwa maswali.

"Hili swali limetushinda, limewashinda hata wakongwe wa historia ya maisha ya Yesu, wakiwamo Wayahudi wenyewe, huenda siku nzuri ya kupata jibu na tutakapomuona Mwenyewe," ameongeza.

# Kalenda ya Gregory na Kumbukizi ya 440

**Na Mwasiende KIZINGE**

MWAKA 2022 ni kumbukizi ya 440 ya "Kalenda ya Gregory," iliyotangazwa mwaka 1582 na Papa Gregory XIII.

Kabla ya "Kalenda ya Gregory," ulimwengu umekuwa na kalenda nyingine nyingi. Mfano, kumekuwa na Kalenda ya Wachina, Wamisri, Wagriki, na Waarabu.

Kalenda hizi zilitumiwa katika kugawanya na kutawala rasilimali ya muda. Hivyo, kumbukizi hii ni nafasi muhimu kwa ajili ya kutafakari nafasi ya "kalenda" katika maisha yetu.

Kihistoria, "Kalenda ya Gregory," ilitangazwa mwaka 1582, na kuchukua nafasi ya "Kalenda ya Julius Kaizari," iliyokuwa imetangazwa tangu mwaka 46BK.

Sababu kuu ya kukarabati "Kalenda ya Julius" ilikuwa ni kuondoa utata kwenye tarehe ya Sikukuu ya Pasaka. Kihistoria, Sikukuu ya Pasaka , iliyo utambulisho wa Ukristo, lazima ifanyika siku ya Jumapili baada ya Sikukuu ya Kutoka (Passover), iliyo utambulisho wa Uyahudi. "Kalenda ya Julius" ilikuwa inavunja kanuni hili.

Kimabadiliko, Papa Gregory alifanya marekebisho kadhaa. Kwanza, alifuta siku 10 za mwaka 1582 kusudi Alhamisi ya Oktoba 4, 1582 ilifuatiwa na Ijumaa ya Oktoba 15, 1582.

Pili, aliamua kwamba, kila mwaka usiogawanyika kwa namba "nne" uwe na siku 365, yaani mwaka mfupi; na kwamba, kila mwaka unaogawanyika kwa namba "nne" uwe na siku 366, yaani mwaka mrefu; kusudi, kwa wastani, kila mwaka ulio katika "Kalenda ya Julius" uwe na siku 365.25.

Tatu, aliamua kwamba, miaka ya kikarne, yaani miaka inayoishia na zero mbili na isiyogawanyika kwa 400, iwe ni miaka mifupi; wakati miaka ya kikarne na yenye kugawanyika kwa 400, iwe miaka



*Kalenda*

mirefu.

Kwa hiyo, katika "Kalenda ya Gregory," ndani ya kila karne nne baada ya mwaka wa kikarne, kuna siku 146,097 zinazopatikana kwa kuzidisha siku 365.25 mara siku 400 na kisha kutoa siku tatu.

Kwa njia hii, mwaka wa "Kalenda ya Gregory" unazo siku zinazotokana na kugawanya siku 146,097 dhidi ya siku 400 na hivyo kupata siku "365.2425."

Kimaudhui, "Kalenda ya Gregory" imegawanyika kwenye siku yenye saa 24, wiki yenye siku saba, miezi minne yenye siku 30, miezi saba yenye siku 31, mwezi wa Februari wenye siku 28 katika mwaka mfupi, mwezi wa Februari wenye siku 29 katika mwaka mrefu, na mwaka wenye wastani wa siku 365.2425.

Kimuundo, "Kalenda ya Gregory" inaonyesha siku kama mzunguko wa saa 24; wiki kama mzunguko wa siku saba; miezi kama mzunguko wa siku 29.5 kwa wastani; na mwaka kama mzunguko wa siku 365.2425, kwa wastani. Wamisionari ndio walituletea "Kalenda ya Gregory." Inatuacha huru kwa kiasi gani kama Taifa? Tafakari.

# Tanzania iamue kuwa tajiri

**Na Godwin Chilewa, Texas, Marekani**

KILA Jimbo la Marekani kuna vivutio lukuki vinavyosaidia kuingizia mapato serikalini; kila ziwa, kila mto, kila bonde la kupendeza au msitu, ni chanzo cha mapato.

Viko vituo vya makumbusho ya kila kitu; kuanzia vifaa vya anga, bahari, sayansi, sanaa, jeshi na silaha zake (manowari, vifaru na mizinga) na hata ujasusi (Spy Museum). Hivi vyote ni vyanzo vya mapato.

Mapato haya, yakichanganywa na kodi mbalimbali zinazokusanywa, huiwezesha serikali kugharimia miradi mikubwa na kuondoa tozo lukuki kila mahali. Kwa mfano, serikali hutoa kompyuta mpakato bure kwa wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari.

Nimeelezea haya yote ili kuonesha haja ya Serikali ya Tanzania kufikiria na kubuni vyanzo vipya vya mapato, badala ya kuwatoza wananchi maskini fedha kidogo walizonazo kwenye miamala ya simu.

Tanzania inavyo vivutio vingi ambavyo kama vikihuishwa vinaweza kutoa ajira kwa wananchi na kuwafanya wao wazirudishe serikalini kwa furaha kupitia matumizi yao. Wananchi wa Tanzania ni watumiaji wazuri sana wa fedha, na kama huamini angalia idadi ya watu waliotembelea Viwanja vya Maonyesho ya Sabasaba kila mwaka na wale wanaohudhuria viwanja vya mpira kuangalia soka.

Kama watu wanaweza kutembelea mabanda ya Sabasaba, siyo ajabu kuwa wanaweza kutembelea vivutio vingine vya ndani kama vikijengwa na wakihamasishwa kufanya hivyo. Leo hii mtu akitembelea jijini Dar es Salaam, hana sehemu nyingi za kutembelea kwa kujifunza. Zamani kila mtu alikwenda soko la Kariakoo maana lilionekana ndiyo muujiza. Leo hii limekuwa kitu cha kawaida sana.

*Nembo ya TRA*

Ndiyo maana najiuliza, kwa nini jeshi la Wananchi wa Tanzania hawafungui eneo kubwa la makumbusho jijini Dar es Salaam kuonesha silaha mbalimbali zilizotumika kumng'oa nduli Iddi Amini. Nina hakika huo ungekuwa mradi mkubwa wa kuliingizia mapato jeshi, kuwafundisha vijana wetu historia, na kuwajaza uzalendo na kiu ya kulitumikia Taifa kwa dhati.

Au kwa nini chuo kikuu cha sayansi na Tiba Muhimbili hakijengi makumbusho ya sayansi na tiba kwa ajili ya kuwaonesha vijana na wazee wetu mfumo wa mwili wa binadamu ulivyo, na kuelekeza jinsi madaktari wanavyotumia sayansi katika kuokoa maisha ya watu?

Haya ndiyo huwa wanayaonesha kwenye mabanda ya Sabasaba? kwa nini kisijengwe kituo ambapo wanafunzi wanaotamani kuwa madaktari kutoka kila kona ya Tanzania, wanaweza kutembelea kwa kulipa kiasi fulani cha pesa? Tunashindwa nini? Mbona wenzetu wanafanya na wanaingiza pesa?

# Pambazuko

## Gazeti la Pambazuko sasa kupokea matangazo

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii: **0744 768 263** au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

***Karibu sana Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua***

***huduma na biashara yako.***

# Magonjwa ya akili bado tishio

**Na Tryruckia MFINANGA**

HIVI sasa habari kubwa zinazojaza kurasa za magazeti, muda mrefu kwenye redio na televisheni na kufurika kwenye mitandao ya jamii, ni zile zinazohusu wapenzi kuua ama kujeruhi.

Tatizo linakuwa kubwa kila uchao na wengi wenye imani za kidini wadai shetani, "ameongeza nguvu," lakini kwa hakika ni kuwepo kwa ongezeko la magonjwa ya akili.

Wataalamu wa afya na madaktari bingwa wa magonjwa ya akili, wanakiri kwamba Tanzania imekuwa kinara wa matukio yenye dalili kwamba watu wanaokabiliwa na magonjwa ya akili wameongezeka.

Mabingwa wa magonjwa hayo wanaeleza kwamba magonjwa ya akili ni matatizo ya ubongo ambayo humfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii na kushindwa kukabiliana na changamoto za maisha.

Kwamba magonjwa ya akili yanaweza kusababishwa na sababu mbalimbali ambazo wataalamu hao wanazigawanya katika makundi mawili; kibaiologia au kisaikolojia, huku msongo wa mawazo ukitajwa kujumuishwa.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza kwamba usaidizi wa kisaikolojia kwa watu waliokumbwa na kiwewe au msongo wa mawazo upatiwe umuhimu ili kupunguza madhara yatokanayo na ugonjwa huo.

WHO katika takwimu zake za hivi karibuni zaidi, inaonyesha kwamba duniani kote mtu mmoja kati ya watu 10 ni mgonjwa mtarajiwa wa magonjwa ya akili, hivyo kuzitaka serikali kutumia rasilimali kuelimisha na kutibu magonjwa hayo haraka.

Mtetezi wa haki za binadamu, Godlisten Malisa anaeleza kuwa hivi sasa habari za watu kujiua au kuua kwa sababu ya mapenzi au ugumu wa maisha ni kubwa nchini Tanzania na sababu kubwa ni kuwepo kwa ongezeko la matatizo ya akili.



*Mwenye msongo wa mawazo*

"Kujiua kwa sababu ya matatizo ni kuwaachia matatizo makubwa zaidi uliowaacha, iwe mke na watoto au ndugu wa karibu kwani wanaenda kukabiliana na changamoto nyingi za maisha baada ya mtu kujiua, kuliko changamoto walizokua nazo kabla," anaongeza.

Anasema, ikiwa mtu anaipenda familia yake; mkewe, watoto, na ndugu, kamwe asijiue. Kujiua ni ubinafsi. Kujiua ni njia rahisi ya kumaliza matatizo yako, lakini kuacha matatizo makubwa zaidi kwa ndugu na marafiki. Na Kuongeza "kujiua ni kuacha alama ya maumivu isiyofutika kwa familia."

Anashauri kwamba matatizo yakimzidi mtu, ni vyema akahakikisha anashirikisha watu wake wa karibu hata kama hawana uwezo wa kuyatatua – kwani kufanya hivyo, ni mwanzo wa kuepuka kuchukua uamuzi mbaya.

# Anavyopatikana mtoto wa kike, kiume

**Na Deusdedith KAHANGWA**

WALIMU wa bayolojia wanatufundisha kuwa, kwa wastani uwiano wa kupata watoto wa kiume na watoto wa kike ni takribani asilimia hamsini kwa hamsini.

Hata sensa ya watu ya mwaka 2022 nchini Tanzania inaweza kuthibitisha, maana wanawake ni asilimia 51.

Lakini, kuna swali walimu wetu hawajatupa jawabu lake. Pale mtoto, kama vile Juma, anapozaliwa mvulana badala ya kuzaliwa msichana, kama alivyo Amina, uamuzi huo hufanywa na nani?

Sayansi inabainisha kuwa jinsi ya mtoto hupatikana wiki saba za kwanza za mimba kama inavyoelezwa hapa chini.


Hatua ya kwanza ni kupatikana kwa jinsi ya mtoto katika ngazi ya kromozomu zilizo kwenye seli za binadamu (chromosome sex).

Kromozomu ni kundi la vinasaba vinavyofanya kazi ya kusimamia michakato ya mfumo mmojawapo mwilini, kama vile mfumo wa chakula, hewa, damu, figo, neva, na uzazi.

Ndani ya kila kromozomu kuna vinasaba vinavyobeba taarifa za jinsi ya kufanya kazi hizo. Kuna vinasaba vipatavyo 21,000 katika mwili wote. Vinasaba vipatavyo 1,000 vinaratibu kazi za mfumo wa uzazi.

Ieleweke kuwa kromozomu huanza kazi wakati mbegu inaporutubisha yai. Kwa kawaida, mbegu na yai ni seli zenye kromozomu 23, kila moja. Wakati wa urutubisho, mbegu huungana na yai kuunda seli moja kubwa, iitwayo “kijusi,” yaani mimba mpya, yenye kromozomu 46.

Seli hii hugawanyika hatua kwa hatua hadi kuunda mtoto kamili, mwenye seli nyingi, ndani ya miezi tisa, kila seli ikiwa na kromozomu 46. Kila seli ya mtoto huyu huwa na kromozomu zilizopangwa kwenye jozi 23.



*Mtoto akiwa tumboni*

Katika mbegu ya kiume, kromozomu yenye vinasaba vinavyoratibu kazi za mfumo wa uzazi huitwa kromozomu aina ya “Y,” wakati kromozomu zingine ni aina ya “X.”

Na katika yai la kike, kromozomu inayoratibu kazi za mfumo wa uzazi ni kromozomu aina ya “X,” na kromozomu zingine ni za aina ya “X” pia.

Kwa hiyo, mtoto wa kiume huwa na seli za kimwili zenye kromozomu 44 zinazoratibu michakato ya jumla mwilini, na kromozomu mbili zinazoratibu kazi za mfumo wa uzazi. Yaani, kuna kromozimu zenye mfumo wa “44XX+XY.” Kifupi tunaandika hivi: “46XY ME.”

Vivyo hivyo, mtoto wa kike huwa na seli za kimwili zenye kromozomu zilizopangwa kwenye mfumo wa “44XX+XX.” Kifupi tunaandika hivi: “46XX KE.”

Katika hatua hii ya kwanza, mimba inakuwa na mfumo wa uzazi usiofungamana na upande wowote. Ni mfumo wenye sehemu tatu: gonadi mbili zisizofungamana na upande wowote wa kijinsi, au tuseme gonadi huria mbili (bipotential ginads); mifereji miwili ya Muleria (Mellerian ducts) na mifereji

*Endelea Uk. 18*

# Anavyopatikana mtoto wa kike, kiume

*Inatoka Uk. 17*

miwili ya Wolfi (Wolfian ducts).

Gonadi huria na mifereji yake huweza kugeuka jenitalia za kiume au jenitalia za kike, kwa sababu ya kemikali za kimwili zitakazozalishwa.

Hatua ya pili, hujitokeza katika wiki ya saba ya mimba, na inahusu kupatikana kwa jinsi ya mtoto katika ngazi ya gonadi (gonadal sex).

Katika hatua hii, gonadi huria mbili mbili, ama hugeuka ovari au korodani. Korodani inamaanisha kupatikana mtoto wa kiume, ovary inamaanisha kupatikana mtoto wa kike.

Kinasaba muhimu katika hatua hii ni "kinasaba kinachoratibu jinsi ya mtoto," yaani "kinasaba cha SRY." Hii ni pingili inayopatikana katika ncha mojawapo ya kromozomu ya "Y."

Kazi ya "kinasaba kinachoratibu jinsi ya mtoto" ni kuzalisha kemikali inayobadilisha gonadi huria kuwa korodani. Kemikali hiyo inaitwa "protini inayootesha korodani."

Kama "kinasaba kinachoratibu jinsi ya mtoto" kikifanya kazi yake vizuri, "protini inayootesha korodani" huzaliwa na kuzilazimisha gonadi huria mbili kugeuka korodani, na hivyo, kupatikana kwa mvulana.

Kwa upande mwingine, kukosekana kwa "protini inayootesha korodani" huziruhusu gonadi huria zilizo katika mimba kugeuka ovari, na hivyo, kupatikana kwa binti.

Hivyo, mtoto akizaliwa mwanaume kamili anakuwa na mfumo wa kromozomu wenye fomati ya "XY" ulioambatana na "uwepo" wa "kinasaba cha SRY." Yaani, kwenye ngazi ya kromozomu, anakuwa na jinsi yenye fomati ya "46XY ME, SRY+."

Kwa upande mwingine, mtoto akizaliwa ni mwanamke kamili anakuwa na mfumo wa kromozomu wenye fomati ya "XX" ulioambatana na "ukosefu" wa "kinasaba cha SRY." Yaani, kwenye ngazi ya kromozomu, anakuwa na jinsi yenye



*Mimba*

fomati ya "46XX KE, SRY-."

Na hatua ya tatu ni kupatikana kwa jinsi ya mimba katika ngazi ya jenitalia na viungo kadhaa vya mwili, na hivyo kuipa mimba jenitalia zinazoonekana (genital sex).

Katika hatua hii, mimba ya kike hupata jenitalia za nje kama vile "uke" na jenitalia za ndani kama vile "mji wa mimba." Hatua hii husimamiwa na homoni ya estrojeni. Na mimba ya kiume, hupata jenitalia za nje kama vile "uume" na jenitalia za ndani kama vile "tezi dume." Hatua hii husimamiwa na homoni ya testosteroni.

Kwa hiyo, "mwanamume," kama vile "Adamu," ana mfumo wa kromozomu wenye fomati ya "46XY ME, SRY+" na jenitalia za kiume. Naye mwanamke, kama vile "Eva," ana mfumo wa kromozomu wenye fomati ya "46XX KE, SRY-" na jenitalia za kike.

Hivyo, kisayansi, mwanamke hawezi kupatikana kwa njia yoyote ile isipokuwa kukutana na kuungana kwa mbegu za kike na kiume na kutengeneza mtoto.

Katika suala hili, ushirika wa wafuasi wa ukweli usiopigiwa kura (realism) na wafuasi wa ukweli unaopigiwa kura (constructivism) unavunjika, na kunahitajika msuluhishi wa migogoro ya kimataifa.

# Wasomi wetu wanatuangusha

**Mhariri,**

**E**LIMU ni nyenzo muhimu katika kumkomboa mwanadamu katika nyanja zote za kimaisha. Elimu siyo tu kuingia darasani na kusoma vitabu, bali ni kuwa na upeo mpana wa kuchanganua mambo yanayotokea katika jamii.

Elimu makini na sahihi ni lazima imfanye mhitimu kuenzi tamaduni nzuri zilizopo katika jamii inayomzunguka. Msomi ni mtu anayepaswa kuigwa kwa matendo yake yenye hekima katika jamii. Katika nchi yetu wasomi wengi "hawajisomi" na baadhi yao wamekuwa wakiishi mithili ya wanyama kwa kutotumia elimu yao katika kudadisi mambo.

Ni watu wasiofuata na kuheshimu utamaduni wa Kitanzania badala yake, wanasujudia utamaduni wa kigeni usiokuwa na manufaa kwa wanajamii.

Kitambo nilifikiri kwamba elimu ingekuwa silaha nzuri sana kwa Mtanzania kujikomboa kifikra za kiutamaduni, lakini wapi. Elimu ndio imekuwa chombo cha kumfanya msomi kutojitambua kabisa.

Leo hii wasomi wengi hasa wa vyuo vikuu baada ya kupata elimu, sasa wamepata nafasi ya kutembea nusu uchi kwa madaha. Wamepata nafasi ya kuchubua ngozi kwa mikorogo mikali ili kufanana na mzungu.

Niliwahi kuandika makala mbili katika moja ya magazeti nchini Desemba, mwaka 2010, chini ya kichwa cha habari "hawa ndio wasomi wetu wa leo" na "kama huu ni uongo ukweli ni upi" nikieleza hisia zangu juu ya mmomonyoko mkubwa wa maadili miongoni mwa wanazuoni wetu, baada ya kupata nafasi ya kujiunga na chuo kikuu. Katika hali isiyotarajiwa, baadhi ya wanachuo waliopata kusoma makala zile walinishambulia kwa matusi na kunikejeli.

Nilifikiri kuwa nimekosea lakini leo hii nimejiridhisha kwa uchunguzi niliofanya na kukiri kuwa wengi wa wasomi wetu ni chachu ya mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu. Ni wasomi ambao wanapenda kusoma habari nyepesi katika magazeti ya udaku badala ya kutafuta habari muhimu ambazo ni za uhakika. Ni wavivu wa kusoma majarida na vitabu. Waangalie vijana wanaosoma katika taasisi mbalimbali za elimu wengi wao wanawaza kujilimbikizia mali pindi wanapopata nafasi za kazi au utawala waanze kula mpaka waote vitambi. Wanawaza kuwa wezi wa mali ya umma na kuwa mafisadi hata kabla hawajapata fursa hizo maridhawa. Sasa wakipata itakuwaje?

Kwa nchi kama hii yenye wananchi masikini, kama kila msomi atawaza kujilimbikizia mali kamwe hatutafikia maendeleo. Maendeleo dhaifu katika nchi yetu ni matokeo ya Watanzania hasa wasomi kutanguliza maslahi yao binafsi kuliko ya jamii kwa ujumla.

***Elifuraha John,***
***jogofefu@yahoo.com***

## *Tunapokea Barua*

***Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: info@pambazuko.tz au kupitia namba ya simu: 0744 768 263***

# Falsafa ya ustawi wa binadamu

**Na Mwandishi WETU**

PROFESA Germain Grisez na wenzake wa Marekani, hasa katika kitabu chao, "Beyond the New Morality: The Responsibilities of Freedom (1988)," sura ya saba, wameongea kuhusu "ustawi ni kitu gani na siyo kitu gani." Wanaongelea tunu nane ambazo hapa zimegawanywa baadhi na kuzalisha tunu 12 kwa ujumla. Nazijadili hatua kwa hatua.

Maisha (life) ni tunu inayohusiana na uwezekano wa mtu, kama mnyama mwenye mwili uhai, kuzaliwa, kukua, na kuzeeka hadi kifo asilia.

Uzazi (procreation) ni tunu inayohusiana na uwezekano wa mtu, kama mnyama mwenye mwili wa kijinsia, kuona sababu ya kujumuika kingono ili kuzaa na kuendeleza ukoo wake.

Afya (health) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mnyama mwenye mwili hai unaoshiriki katika matendo ya kila siku, kuona sababu ya kutunza na kulinda maisha yake dhidi ya magonjwa ili aweze kutimiza majukumu yake ya kila siku.

Maarifa (knowledge) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye mwili, akili na utashi, kutafuta ukweli na kuutumia kuyamudu mazingira yake.

Urembo (aesthetic experience) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye mwili, akili, utashi, na hisia kufurahia urembo asilia na kuboresha maumbile kwa njia ya mapambo.

Kazi (excellence in work) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye mwili, akili, utashi, kuustaarabisha ulimwengu kwa kwa njia ya kazi za kiakili na kimwili.

Burudani (excellence in play) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye mwili, akili, utashi, kubuni na kushiriki kwenye shughuli za burudani kwa ajili ya kufurahisha nafsi yake.



*Prof. John Danaher*

Ndoa (marriage) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mnyama mwenye mwili wa kijinsia, kuanzisha ndoa, ikiwa inatabulishwa na tendo la ngono, ambalo linaweza kuwa sababu, na hivyo, alama asilia ya umoja wa kikemia, uzazi, utulivu wa moyo, uaminifu, na udumifu.

Urafiki (friendship) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye akili na utashi, kuchagua amani na kuepuka migogoro kati yake na majirani zake.

Utulivu wa moyo (self-integration) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye akili na utashi, kuchagua amani na kuepuka migogoro kati ya matawi mbalimbali ya nafsi yake.

Busara (practical reasonableness) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye akili na utashi, kuchagua amani na kuepuka migogoro kati ya fikra, maamuzi na matendo yake.

Na dini (religion) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu, kama mtendaji mwenye akili na utashi, kuchagua amani na kuepuka migogoro kati yake na ulimwengu wa roho.

# Tunu za vigezo vya maendeleo

**Na Mwandishi WETU**

WASOMI wengi duniani wameandika sana kuhusu maana halisi ya maendeleo. Miongoni mwao ni Profesa Martha Nussbaum wa Marekani.

Profesa Martha ameandika kwa kuhoji kuhusu "maendeleo ni kitu gani na siyo kitu gani," katika kitabu chake, "Creating Capabilities: The Human Development Approach (2011)," kwenye ukurasa wa 33 hadi 34.

Anajadili tunu kumi. Katika makala haya nimezigawanya na kuzalisha tunu 12 kwa ujumla. Nazijadili hatua kwa hatua. Kwa mujibu wa Nussbaum:

Uhai (life) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kuishi maisha marefu hadi kifo cha uzeeni; pasipo kufa kabla ya wakati kwa sababu holela za kimazingira.

Afya ya mwili (bodily health) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kuwa na mwili na akili thabiti vinavyomwezesha kutekeleza majukumu yake ya kiuchumi na kijamii, ukiwemo uwezo wa kupata chakula bora na makazi bora.

Ukamilifu wa kimwili (bodily integrity) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kujongea na kufika atakako; kuwa huru dhidi mashambulio ya kimwili, kupata faraja ya kimapenzi, na kuamua lini awe mzazi.

Uhuru wa kufikiri na kueleza fikra binafsi (freedom of thought and expression) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kutafakari na kujieleza kama binadamu mwenye maarifa kamili yatokanayo na mafunzo thabiti ya kielimu.

Afya ya hisia (emotional health) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kupenda, kupendwa, kusamehe, kuhuzunika, na kushukuru, bila hofu ya kulaumiwa na yeyote.

Busara (practical reason) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kutofautisha mema na mabaya, mbinu na malengo, na hatimaye, kufungamanisha mbinu na malengo aliyojiwekea kwa



***Prof. Martha Nussbaum***

ufanisi.

Kujumuika na wengine (social affilliation) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kukusanyika na kujumuika na wenzake kwa uhuru.

Kuheshimiana kama watu (dignified affiliation) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kutodhalilishwa utu wake kwa kubaguliwa kwa misingi ya rangi, jinsi, nasaba, ukoo, dini, au asili ya utaifa.

Kufungamana na mazingira asilia na bayoanwai (relationships with the world of nature and other species) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kuishi kwa kujali nafasi ya wanyama, mimea na mazingira asilia katika maisha yake.

Burudani (play) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kucheka, kucheza na kufurahia shughuli za burudani.

Kutawala mazingira ya kisiasa (control over one's political environment) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kushiriki kikamilifu kwenye uamuzi wa kisiasa unaogusa maisha yake.

Na kutawala mazingira ya kiuchumi (control over one's economic environment) ni tunu inayohusiana na uwezo wa mtu kumiliki mali; kutafuta na kupata ajira bila ubaguzi wala ukatili wowote.

# Katiba na vigezo vya maisha bora

**Na Deusdedith KAHANGWA**

NENO "haki" linamaanisha mambo matano kwa mpigo. Kwanza, kuna kitu cha thamani, yaani "tunu," inayopaswa kulindwa, kuheshimiwa na kutimizwa na mtu baki, haya yakiwa ni "madai" stahiki.

Pili, kuna mtu ambaye ni "mleta madai." Tatu, kuna mtu ambaye ni "mbeba jukumu" la kutekeleza madai. Nne, kuna "kitendo" kinachopaswa kutekelezwa au kuachwa kutekelezwa na mbeba jukumu ili madai yatimie. Na tano, kuna "sababu," yaani kanuni ya kimaadili au ya kisheria, inayohalalisha madai husika.

Chukulia "haki ya kufanya kazi." Madai ni ujira halali; mleta madai ni mfanyakazi; mdaiwa ni mwajiri; jukumu la mdaiwa ni kulipa ujira halali; sababu ya madai ni kazi iliyofanywa kwa mujibu wa mkataba. Lakini, bado hatujataja "tunu" husika.

Hiyo "haki ya kufanya kazi," ni kanuni ambayo ni nyenzo ya kulinda tunu za msingi kama vile uhai wa mwajiriwa, uhai wa familia yake, elimu ya watoto wake, fursa za kuburudika, kuabudu, kukusanyika, amani ya moyo, ujirani mwema, na tunu baki kama hizo, ambazo ni tunu za msingi.

Kwa hiyo, kutamka "haki za binadamu" kwenye katiba bila kubainisha "tunu" za msingi zinazopaswa kulindwa na "haki" hizo ni sawa na kutengeneza katiba hewa.

Ni kwa sababu hii tunasema kuwa, mwaka 1961, Tanganyika ilipopata uhuru ni sawa na kuuziwa mbuzi mwitu kwenye gunia, maana katiba ile haikutaja haki za binadamu.

Taratibu, katiba hii ilifanyiwa mabadiliko kadhaa. Mwaka 1962 ikawa Katiba ya Jamhuri, mwaka 1964 ikawa katiba ya Muungano; mwaka 1977 ikaimarishwa na kuwa katiba ya kudumu; na mwaka 1984 ikawa katiba ya "haki za binadamu."

Haki hizi ni kanuni za kimaadili ambazo ni nyenzo za kulinda "tunu" za msingi za binadamu kwa kuruhusu na kukataza matendo fulani. Lakini, "haki" zilizotajwa kwenye katiba yetu hazijakamilika hadi leo. Tulisahau kutaja "tunu" za msingi zinazopaswa kulindwa na haki hizo.



*Prof. Amartya Sen*

Ni katika mazingira haya, mwanafalsafa na mchumi wa huko Singapore, profesa Amartya Sen, kupitia kitabu chake kiitwacho, "Commodities and Capabilities (1985)," aliamua kuiuliza dunia swali gumu.

Hakuwa anafurahishwa na tabia ya serikali za dunia kupima kiwango cha maendeleo kwa kutumia kigezo cha mali na kipato, bila kujali mali na fedha zinatumika vipi kuboresha maisha ya mmiliki husika.

Hivyo Sen akauliza: Kwa mujibu wa vigezo vyetu vya kupima maendeleo, maisha bora ni kitu gani na siyo kitu gani? Na huyu, Amartya Sen, ndiye mwanafalsafa wetu wa wiki kwa leo.

***Tutafakari pamoja naye.***

# Tumuombee heri Fei Toto



Na Shaaban LULELA

MENGI yanaweza kusemwa kuhusu mpira wa miguu kwa timu za Tanzania, lakini yote hayawezi kukamilika bila kutaja timu kubwa mbili zenye historia nchini humo; Simba na Yanga.

Sababu za kutoachwa kwa timu kwenye historia ya mpira huo kwa Tanzania zipo nyingi, zaidi ya 1000 – ingawa kubwa ni kuhusishwa na idadi kubwa ya mashabiki, ukwasi, mbinu kali za ushidi – ndani na nje ya uwanja.

Kama ilivyokuwa kwa timu, pia kwa wachezaji – kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, huwezi kutaja wachezaji watatu bora kwenye Ligi Kuu ya Soka Tanzania, kamuacha Feisal Salum, maarufu – Fei Toto wa timu ya Yanga.

Sifa za Fei Toto zipo ndani ya uwanja kama ilivyo awapo nje ya uwanja. Ni pole, mwelewa, hana papara na anaweza kumudu vyema kila hatua ya ushauri wa maana.

Akiwa uwanjani, upole wake ni uleule – anatoa pasi kwa umakini mkubwa kama anavyopokea, anaelewa wakati gani ampe nani mpira ili aweke kimiani, anaweza kupiga chenga za maudhi na anasikiliza wenzake, akiwamo mwalimu na wasaidizi wengine.

Ni kutokana na sifa hizo, Fei Toto amekuwa akitajwa mara kadhaa kuhamia timu nyingine kubwa zaidi. Siyo mara moja ama mbili, timu yake imesikika ikieleza anavyowindwa na timu za nje ili akafanye majaribio huko na ikiwezekana kununuliwa kabisa.

Sasa huenda hayo yakatimia hivi karibuni, ukiacha kwamba anaelezwa kutamani kuanza kuvaa jezi za timu nyingine kubwa – Azam, Fei Toto anakaribia kabisa kwenda kufanya majaribio Uingereza.

Pamoja na kwamba haijawekwa wazi, lakini Pambazuko limefahamishwa kwamba ni suala la muda tu, kila kitu kitakuwa hadharani. Kwamba Fei Toto sasa atasafiri kwenda kucheza timu ya Uingereza.

Mwandishi mmoja wa michezo, hasa soka, Oscar Oscar amewahi kumwelezea Fei Toto kuwa ni mchezaji mwenye sifa kubwa tatu; Fei anafurahia kucheza mpira. Huwa hachezi mpira kwa hasira na hana papara. Hateseki mpira unapokuwa miguuni kwake na hauogopi.

Mmoja wa watu wa karibu zaidi na Fei Toto alipoulizwa na Pambazuko kuhusu tetesi hizo za kwenda Uingereza, hakuwa na maneno mengi zaidi ya kueleza kuwa – “ni kweli jambo hilo lipo, kama halipo basi linakuja.”

***Kila jema kwa Fei Toto.***

# MAMA KAZINI



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuashiria kuanza kwa hatua ya kuruhusu kuanza kujazwa kwa maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) kwenye Mto Rufiji mkoani Pwani wiki iliyopita – Desemba 22 Desemba, 2022 (Picha na Ikulu).*

*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION